

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
MAHAKAMA YA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU DIVISHENI YA KAZI**

**KANDA YA DAR ES SALAAM**

**MAOMBI YA ANUAI NA. 704 OF 2019**

**GUY ALBERT KITWANGE 37 OTHERS....MUOMBA MAREJEO**

**VERSUS**

**ISMAIL HOTEL.....MJIBU MAREJEO**

**UAMUZI MDOGO/RULING**

*Tarehe ya mwisho ya Amri: 19/02/2021*

*Tarehe ya Uamuzi mdogo/Ruling: 31/03/2021*

**Z. G. Muruke, J.**

Guy albert na wenzake 37, walikuwa waajiriwa wa Ismail Hotel. Hawakuridhika baada ya kuachishwa kazi walifungua mgogoro tume kupinga uamuzi. Tume ilitupilia mbali maombi yao kwa kukosa mashiko. Walifungua marejeo namba 57/2019 ambayo yaliondolewa yakiwa na ruhusa ya kurejesha ndani ya siku 30 toka tarehe ya kukubaliwa kesi ya uwakilishi. Nimepitia kiapo kinachounga mkono hoja, kiapo pingamizi na maelezo ya kina ya wawakilishi wa waleta maombi na wajibu maombi. Sababu zilizotolewa na waleta maombi ni kwamba wametapaka maeneo mengi, hivyo kuwa kikwazo kupata saini zao wote hivyo kuchelewa. Ikumbukwe kwamba, waleta maombi wanaomba waongezewe muda ili kuleta ombi stahiki. Hii ni haki ya kutaka kusikilizwa ambayo ni muhimu sana. Kwa mantiki hiyo sioni sababu za kutoridhia. Waleta maombi

wamekubaliwa ombi la kufungua shauri la uwakilishi nje ya muda.  
Wafungue ndani ya siku 30 toka tarehe ya leo. Imeamiriwa hivyo.




Z.G.Muruke

**JAJI**

31/03/2021

Uamuzi huu umetolewa leo mbele ya Guy Albert na Ramadhani Athumani  
wawakilishi wa waleta maombi wajibu maombi hawapo.



Z.G.Muruke

**JAJI**

31/03/2021

